

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA



5/5/2022

TANGAZO

TANGAZO LA ZABUNI YA USAFISHAJI WA MJI , UZOAJI WA TAKA NGUMU PAMOJA NA UKUSANYAJI WA TOZO YA ADA YA USAFISHAJI WA MJI.

1. Halmashauri ya muheza inawatangazia makampuni kuwa inahitaji kupata wazabuni wenye uwezo wa kusafisha mji , uzoaji wa taka ngumu pamoja na ukusanyaji wa tozo ya ada ya usafishaji wa mji kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa sheria ndogondogo za Halmashauri kama ilivyoainishwa hapo chini:-

ZABUNI NAMBA	JINA LA ZABUNI
LGA/132/2021/2022/G/39	UWAKALA WA UKUSANYAJI ADA YA UZOAJI WA TAKA NGUMU PAMOJA NA KUZOA TAKA
	1. KATA YA MASUGURU 2. KATA YA TANGANYIKA 3. KATA YA GENGE 4. KATA YA MBARAMO 5. KATA YA MAJENGO 6. KATA YA KWAMKABALA

3. Masharti kwa Waombaji:-

Mwombaji awe na uwezo wa kusafisha mji wa Muheza ikiwa ni pamoja na kuzoa taka zote na kuzipeleka kwenye eneo la Dampo Kitisa.

- i. Mfumo wa kielektroniki unaotumika na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ni Local Government Revenue Collection Information System – LGRCIS kwa ajili ya kukusanya ada ya tozo ya uzoaji taka.
- ii. Tozo ya ada itakayokusanywa itaingizwa katika Akaunti ya Halmashauri na wakala atalipwa baada ya kuwasilisha hati ya madai . Muda wa malipo kwa wakala ni ndani ya siku saba [7] ya mwezi unaofuata baada ya wakala kuleta hati ya madai husika.
- iii. Wakala atatakiwa kuonyesha kiwango cha asilimia atakachoipatia Halmashauri baada ya kutoa gharama zake za uendeshaji pamoja na faida
- iv. Muombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri
- v. Muombaji awe na Leseni hai ya Biashara
- vi. Muombaji awe na usajili wa kuandikishwa kwa Kampuni
- vii. Muombaji lazima atoe mchanganuo wa namna atakavyofanya usafi mji wa Muheza.(ambatanisha mchanganuo)
- viii. Muombaji awe na "Taxpayer Identification Number(TIN)"
- ix. Muombaji aonyeshe uthibitisho wa kulipa kodi(TAX CLEARANCE)

- x. Asilimia 20% itatozwa kwa wakala atakaye chelewesha marejesho yake ndani ya siku 5 kulingana na tarehe ya marejesho ya mkataba.(ambatanisha barua ya kukubali)
- xi. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (**Power of attorney**) wa mtu atayehusika na zabuni hii.
- xii. Muombaji hatakiwi kuwa mtumishi au Kiongozi wa Halmashauri ya wilaya muheza.
- xiii. Uzoefu wa wataalamu au wafanyakazi atakao watumia katika kufanya kazi ya kukusanya ushuru kupitia wasifu wa kila mhusika (CV).
- xiv. Wakala atakayeshinda zabuni hii atawajibika kuweka Dhamana ya utendaji kazi (performance bond financial) fedha taslimu, Wakala atakayeshinda zabuni hii atawajibika kuweka Dhamana ya utendaji kazi ya fedha taslimu za miezi mitatu anazotarajia kukusanya kwa mujibu wa memorandam
- xv. Wakala atawajibika kuhakikisha mji wa Muheza unakuwa safi muda wote wa utekelezaji wa mkataba.

JINSI YA KURUDISHA ZABUNI

Zabuni zitatumwa kwenye mfumo wa Taneps